**Shirika la Amo Zanzibar Tours & Safari**

**SERA ENDELEVU 2019**

Shirika la Amo Tour and Safari limevinjari kupunguza athari zake kwa mzingira ili kuhifadhi rasilimali asilia, mila na utamaduni, hivyo kuhakikisha uendelevu wa shughuli zetu. Shirika letu limeupa kipaumbele cha dhati ustawi wa wakaazi na hifadhi ya mfumo wa mazingira wa visiwa hivi pamoja na bara.

Tunafuata utalii unaowajibika, kufanya kazi zetu ili kuboresha maendeleo ya nchi, kiuchumi na kijamii. Kadhalika, kuwafahamisha zaidi wateja wetu zile njia za usafiri zisizo na madhara makubwa, na zinazowafikiana na mazingira.

Yafuatayo ni maelezo ya kina jinsi tunavyolichukulia suala hili, na vile tunavyolitekeleza katika kila nyanja ya utendaji wetu.

## Kauli Mbiu

"Tunaaazimia kutoa utalii muwafaka unaowajibika ili kuwajuvya wageni wetu waelewe vilivyo kuhusu eneo la Mwambao wa Waswahili na sehemu za mjini. Na huku tukipunguza hasi zinazotokana na utalii, pamoja na uharibifu wa mazingira na athari zake kwa jamii.Huu mpango wetu uendelevu unawaelewesha zaidi washirika na wageni wetu umuhimu wa kuhitajika kuhifadhii mila, rasilimali za kitamaduni na za asili kupitia biashara endelevu.

---

### Ahadi zetu kwa utalii endelevu

---

Tumemteua mwenzetu mahsusi aitekeleze sera ya uendelevu kwenye shirika letu .

Tumetengeneza mpango unaofafanua wazi jinsi kudumisha uendelevu wa shughuli zetu.

Sera yetu endelevu inapunguza madhara makubwa kutokana na shughuli zetu. Pia tunaendeleza utalii wa mnamna nyingine, badala ya ule wa mminiko wa watu wengi, ambao unaathari pakubwa (inasikitisha uharibifu wake unavotokea mara kwa mara) kwa jamii, uchumi, utamaduni na mazingira yanayotembelewa na wageni wetu.

Vile vile sera yetu inawajibika na ustawi wa wafanyakazi wetu kwa kuwapa masharti muwafaka yenye vigezo vinavyohakikisha uzima na usalama wao

Uwazi ni jambo tunaolitilia maanani kwetu. Tunapeana fikra zetu na hatua tunazozichukua kuhus utendaji wetu, na washirika wetu wa biashara, wateja na watu kwa jumla.

Tunahakikisha kwamba timu nzima inaelewa na kutii sera yetu ya uendelevu .

Tunashirikiana na wadau wengine ili kufanikisha utalii endelevu utakaonufaisha ukanda huu.

Tunashirikiana na wadau wengine ili kufanikisha utalii endelevu utakaonufaisha ukanda huu.

## 1. Usimamizi Ndani ya Shirika: Sera ya Kijamii na Haki za Wafanyakazi

Tunafuata kikamilifu sera inyotunza uzima wa usalama wafanyikazi kufuatana na sheria.

Mara kwa mara, wafanyakazi wetu wanaelekezwa na kufahamishwa haki na majukum yao, vilevile wajibu wa Shirika juu uzima na usalama, inapotokea, Mungu Atunusuru, moto, maafa ama ugaidi.

Ofisi yetu na kila kwenye magari yetu mna vifaa vya huduma ya kwanza. Tunahimiza na kufadhili wafanyakazi kupata mafunzo ya Huduma ya Kwanza

Tunaheshimu uhuru wa mwajiriwa; wafanyikazi wetu wanaweza kuvunja mikataba yao wakati wowote
kwa kutoa notisi mapema, isiyopungua mwezi mmoja, bila ya kuiingia matatani.

Kila mkataba wa ajira unatoa maelezo sahihi ya kazi, ili wafanyakazi wetu wa baadaye wajue nini cha kutarajia na kile kinachotarajiwa kutoka kwao.

Mshahara umetajwa katika mkataba wa ajira na uko juu ya kiwango cha wastani kufuatana na sheria.

Muda ziada wa kazi unlipwa kufuatana na makubaliano ya pande zote: kati ya mfanyakazi na mwajiri.

Malipo ya likizo ya kila mwaka ya muda wa wiki 4 anapewa kila mfanyakazi; pamoja na likizo ya ugonjwa na ya ujauzito inapohitajika.

Pia tunatoa kazi za kibaruwa kwa saa za zisomfunga mfanyakazi, Kadhalika uwezekano wa kuchukua ofu bila malipo, linapotokea jambo, kama vile m siba au harusi

Tunatoa msaada na fursa za mafunzo, pia kwa elimu ziada kwa wafanyikazi wetu

Tunaajiri watu waliofikia umri wa kuajirika kufuatana na sheria

Tunawazowesha wafanyakazi wetu wawasilane kwa uwazi na shirika zima; ili kupunguza msuguano, hasara; na kuhakikisha utendaji wa hali ya juu, ari na ufanisi haushuki kwango chake

Wafanyakazi wanajuvywa utaratibu  na nidhamu za kazini

Amo Zanzibar Tours & Safari inatoa fursa kwa wanafunzi wa kitaifa na kimataifa  wajiunge na shirika,  kwa mafunzo,  kwa muda tu

Tunatoa nafasi za kazi kwa watu wanaokabiliwa na changamoto kila inapowezekana.

Tumepiga marufuku aina yoyote ya ubaguzi wa rangi, kijamii, wasiojiweza, mtu na mwelekeo wake wa kijinsi na kidini…wakati wa kuajiri na katika  Shirika

## II. Usimamizi wa Ndani: Sera ya Mazingira

---

- Kutunza mazingira yetu na maliasili za Zanzibar kwa busara na kwa kuzingatia hali, ili kupunguza madhara. Vifuatavyo ni viwango na mwongozo wetu :
- Kupunguza matumizi ya vitu ambavyo hutupwa vikishatumika au vinayotumika mara moja.
- Pendelea kununua vitu vilivyotengenezwa vinavyodumu
- Nunua vitu kwa jumla ili kupunguza kaboni inayotoka wakati wa kuvisafirisha, na pia kupunguza ufungashaji vitu usio wa lazima
- Punguza kupiga chapa kwa printer, na kutumia karatasi, badala yake tumia mtandao ni kwa kuwasiliana
- Kadri uwezavyo, tuma taarifa mtanadaoni, badala ya kupeleka vipeperushi viliyochapishwa
- Kwa uchapishaji usioepukika, tumia karatasi iliyosindikwa na wino safi ukipatikana
- Toa au zima vifaa vya umeme na taa unapokuwa hutumii, badala ya kuviacha tu
- Tumia feni badala ya kiyoyozi
- Tenganisha takataka na risaikil karatasi, vitu vya plastiki na vya vigae
- Fanya risaikil ya betri
- Fanya risaikil ya vifaa vya kielektronik
- Fuata sheria kuhusu makarao na utupaji taka
- Kadri uwezavyo, tumia dawa za kusafishia zinazotunza mazingira. Usitumie tindi kali, (Tuna mtu wetu anayetambulika kwa kutafuta vitu vinavyotunza mazingira)
- Punguza kutumia chupa za plastik kwa wakala nunua chupa 5-1 kupunguza ufungwaji wake uliokithiri
- Nunua vitu vinayotengezwa nchini kupunguza uletwaji/usafirishwaji wake unaopelekea uchafuzi wa mazingira
- Tunza vifaa na mitambo ili kuepusha uharibifu (k.m. maji yanayotiririka)
- Fanya ukaguzi wa mara kwa mara na matengenezo ya magari ya Amo Zanzibar kufuatana na vigezo vinavyotwekwa
- Wasiliana na timu uwaonyeshe upya ufahamu wao jinsi ilivyo muhimu kwa shughuli zetu

## Usimamizi wa Ndani ya Shirika: Mahusiano na Jamii

Kukuza uchumi wa nchi kwa kuwatembeza watalii kwenye maduka madogo dogo, kwa mafundi na kwa wafanyabiashara wa kienyeji

Kutoa mwonekano zaidi wa utamaduni na ufundi wa kienyeji ili kuimarisha utunzaji wa mambo hayo

Kuajiri watembezao wageni, madereva, wafanyakazi wa ofisi na wengineo kutoka kwenye maendeleo. Hivyo kuchangia maendeleo ya kijamii na kiuchumi.

Kushirikiana na wenyeji kutoa huduma kwa wageni wetu; (kama vile kuwaandalia chakula majumbani )

Kuwawezesha wageni wetu wagundue na wajionee mambo yalivyo hasa, siyo ule utalii wa mminiko wa wageni,  na yale "maelezo yasiyo ya kweli"

Wageni wajuvywe kuhusu mila na desturi za wenyeji, ili kukuza uelewa bora na heshima (kama vile mavazi, tabia, hulka n.k)

Kuwalipia   vijana wanaotembeza wageni wapate mafunzo Kawa Training Centre ili kuchangia maendeleo kwenye  msingi wa jamii

Tunalenga hasa wageni wanaokuja wenyewe, familia na vikundi vidogo vidogo ili kukuza utalii unaozingatia  utamaduni na mazingira. Sio ule utalii wa mminiko wa wageni. Kazi yetu ni kuendeleza maingiliano ya dhati  baina ya watu wa utamaduni tofautii, uliojengeka kwa kuheshimana, kuthaminiana  na nia njema.

Huo ndio msingi wetu wa kutunza urithi asilia,utamaduni, utalii, imani na historia yetu.

## IV Wateja Wetu

Tunatoa maelezo yenye kuvutia na kushajiisha juu ya maeneo yanayotembelewa na wageni, kuhusu mila na utamaduni,  pamoja na mazingira halisia.

Kwa taratibu,  tunawajuvya  watu kuhusu athari za utalii, na kujua jinsi ya kutoa njia mbadala iliyo endelevu kabisa; kulingana na ‘’viwango vya utendaji wa utalii wa mminiko wa wageni’’ Kwa upande wa:

Usafiri

Shughuli za kuwafurahisha wageni

Malazi

Kuandaa chakula

Kwenda kununua vitu vya kitalii

Tumeweka wazi kabisa  viwango vya utendaji na mwelekeo wetu.

Tunapanga safari kwa matakwa ya mteja

Tunatoa huduma ya masaa 24 kwa wageni wetu

Tunaheshimu faragha/stara yao wageni wetu

## V. Washirika Wetu

Tunashirikiana na wenyeji, hasa  nwalio kwenye msingi wa jamii ili wao pia wanufaike na wingi wa utalii.

Tunachagua washirika wa biashara ambao wana maadili  kama yetu na waliovinjari kutekeleza utalii endelevu

Kwa kufanya hivyo, tunahakikisha huduma zetu zote ni endelevu kwa kila hatua, pamoja na kuchangia katikahifadhi wa urithi wa maliasili, mila na utamaduni wa nchi.

Tuko pamoja na  washiriki watarajiwa kukuza mbinu endelevu.

Tunafanya kazi na mashirika yanayoheshimu haki za wafanyakazi wao kwa mujibu wa sheria.

Tunankuza uwelewa kwa vikundi ambavyo tuna maslahi mamoja , bodi na mashirika mengine yanayohusika na utalii.

Tumesimama kidete kupinga kuwatumikisha watoto wadogo na utalii unaovunja maadili

## VI. Huduma zetu: Safari na Harakati zetu

Hii ndiyo kazi yetu kuu, na tunaelewa majukumu yake,  pia fursa kubwa inazotupa. Tunajitahidi kuleta  "manufaa kwa pande zote, wateja wetu, wenyeji na kwa mazingira asilia:

Katika safari na shughuli zetu hatuwawapitishi wateja wetu kwenye njia kuu, ili kusawazisha athari za kwa mazingira kwenye maeneo yanayotumiwa kupita kiasi.

Watembezaji wageni wetu hupatiwa mafunzo mara kwa mara ili wawe na ujuzi mkubwa kabisa kadri iwezekanavyo. Kwa sababu wao ndio wanajamii wanaoweza kuwapa wateja wetu maarifa na maelezo ya kina.

Tunatangaza ziara zetu  taratabu kwa wageni. Mtembezaji  huwa na muda wa kuelezea historia, mila, kutoa hadithi kwa makini; pamoja na kuwapa fursa wageni kujaribu mambo, kuliko wakawa wanapita njia wakitupia jicho tu. Kwa kufanya hivyo, wageni hupata uwelewa mambo kwa njia mbadala na iliyo muwafaka.

Tumejenga ushirikiano mzuri na wanakijiji na watu wa mjini. Hivyo huwawezesha wageni kujionea hali halisi na kukutana na watu wenyewe,   utalli wa kwenye jamiii,  badala ya ule wa *‘’kijuu juu ‘’*. Kwa kushirikiana na wenyeji, (wageni huwandaliwa chakula majumbani na familia) Tunaunga mkono jamii, kulliko kwenye sehemu za utalii mkubwa

Safari na shughuli zetu daima hupangwa kukidhi matakwa na vile apendavyo mteja; kuliko kufuata ule mzunguko wa kawaida. Hutembeza wageni kwa vikundi vidogo vidogo,  ili wateja wetu wapate kujionea wenyewe maisha yalivyo hasa; , na, pia,  kupunguza madhara utalii huenda ikailetea mazingira.

Ziara zetu zinawafahamisha wageni kwa busara jinsi ya kuwajibika wanapokuwa safarini

Tunashirikiana na taasisi zinashughlika na kuhifadhi na hali ya mazigira nchini.

Tunawaalika wateja wetu kutembelea miradi midogo dogo inayofanywa na jamii, ambayo ni endelevu kwa mazingira na utamaduni.
Kwa kufanya hivyo, tunaunga mkono juhudi za kuongeza mwonekano wao na mapato. Na pia kukuza utalii mbadala, sio ule  wa  ‘’mminiko wa wageni’’.

Hatukubali pendekezo lolote kuhusu safari au shughuli zozote  zitakazowaletea madhara wananchi  (maelezo yasiyo sahihi,  utalii usio na maadili).

Hatukubali pendekezo lolote kuhusu safari na shughuli zozote zinazoleta madhara kwa wanyama na mimea (wanyama wanaowekwa kizuizini, mawindaji)

Hatukubali pendekezo lolote kuhusu safari na shughuli zozote zitkazowatesa wanaadamu au wanyama

## VIII Huduma Zetu: Usafiri

Tunapendekeza kutumia usafiri  wa pamoja ili kupunguza utokaji wa gesi chafu

Tunajitahidi kupunguza muda barabarani kwa kuchangana matembezi na safari zetu

Tunazipa kipaumbele, kadri iwezekanavyo, fursa nyingine kutembelea maeneo ya ikolojiakuendesha baskeli vilimani, na kupanda mitumbwi n.k)

Tunayataunza vizuri magari yetu, kufuatana kanuni za kudhibiti gesi chafu

---

**IX. Uhifadhi wa Wanyama**

---

Hatushiriki na uovu wowote wanaotendewa wanyama

Hatuungi mkono wanyama wanaofungiwa (isipokuwa kwa ajili ya kuwahifadhi)

Hatuungi mkono ujangili. (Mfano: hatununui vitu vya kumbukumbu ambavyo vinavyohusiana na kitendo hicho) . Hatujirikishi na kitendo chochote kinachohusiana na uwindaji wanyama

Tunaunga mkono miradi ya kuhifadhi wanyama pori, pamoja, na kulinda makaazi yao

Tunawashauri wateja wetu wasinunue vitu vya kumbukumbu ambavyo utengenezaji wake umehatarisha mimea na viumbe

Kustawisha uwelewa na kutafuta fedha za kuwalinda wanyama pori. (Pomboo, Kasa, KIma n.k.) Tunapendekeza kwa wateja wawaangalie wanyama katika makao yao halisia, lakini wasiwatiribue. Tunakataza kabisa kufanya kitu kitachowacharura wanyama, kama kuwalisha au kujaribu kuwagusa.

Tunaendeleza uelewa wa wateja wetu kuhusu haja ya kutunza mazingira na hali ya viumbe hai

______________________________ __________________________________

Amour Suleiman Amour El-Hinawy
Mmiliki mwazilishi
Wa shirika la AMO Zanzibar Tours & Safari

Noreen Cichon
Mkurugenzi Mtendaji
na Mshauri wa Safari za kitalii
Amo Zanzibar Tours & Safari’s Team

7th May 2022